



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA



**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

**04/10/2021**

Kwa mujibu wa kibali cha ajira mbadala kilichotolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora chenye Kumb. Na FA.170/361/01"A"/162 cha tarehe 10/09/2021, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga anawatangazia watazania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi zifuatazo:-

**1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III-NAFASI TATU (3)**

**1.1 Sifa za mwombaji**

Awe na elimu ya kidato cha nne (IV) au sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii, kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**1.2. Majukumu ya Mtendaji wa Kijiki Daraja la III**

- (i) Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiki
- (ii) Kusimamia ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiki
- (iii) Kuratibu na kusimamia upangaji wa Utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiki.
- (iv) Katibu wa Mikutano ya Kamati zote za Halmashuri ya Kijiki.
- (v) Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- (vi) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali
- (vii) Kiongozi wa Wakuu wa vitengo vya kitaalamu katika Kijiki.
- (viii) Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Vijiki

**1.3 Ngazi ya Mshahara**

Kwa mujibu wa ngazi ya Mshahara wa Serikali yaani TGS.B kwa mwezi

**1.4 Masharti ya ajira - (Ajira ya kudumu)**

## 2. DEREVA DARAJA LA II - NAFASI MOJA (01)

### 2.1. Sifa za Mwombaji:

Kuajiriwa mwenye cheti cha Kidato cha nne (Form IV) na leseni ya Daraja la E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari(Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali. Waombaji wenye cheti cha Majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza

### Majukumu ya Dereva Daraja la II.

- (i) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- (ii) Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- (iii) Kufanya matengenezo madogo madogo katika gari.
- (iv) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- (v) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
- (vi) Kufanya usafi wa gari, na
- (vii) Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

### 2.3 Masharti ya Ajira- (Ajira ya kudumu)

### 2.4 Ngazi ya Mshahara

Kwa mujibu wa ngazi ya Mshahara wa Serikali yaani TGS.B kwa mwezi

## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA KILA MWOMBAJI


- (i) Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe na namba ya Utambulisho wa Uraia (National Identification Number) kutoka mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa(NIDA)
- (ii) Muombaji awe na umri kati ya miaka 18-45
- (iii) Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa la jina au kufungwa jela.
- (iv) Maombi yaambatane na wasifu wa mwombaji CV.
- (v) Maombi yaambatanishwe na nakala za vyeti vya elimu, vyeti vya taaluma, cheti cha kuzaliwa Nakala ya leseni kwa madereva na picha ndogo (Passport Size) ya hivi karibuni.
- (vi) Testimonial, Result slip, Provisional Result, kiapo cha kuthibitisha umri wa kuzaliwa **HAVITAKUBALIWA**
- (vii) Barua ya maombi iandikwe kwa mkono
- (viii) Waombaji waliosoma nje ya nchi vyeti vyao vya Taaluma vifanyiwe ulinganifu na TCU na NECTA na majibu ya ulinganisho yaambatanishwe kwenye barua ya maombi ya kazi.
- (ix) Waombaji waliowahi kuacha kazi, kuachishwa kazi au kufukuzwa kazi hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama ana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi cha kuajiriwa upya.

- (x) Kwa waombaji wenye vyeti vya ngazi yaani NTA levels maombi yatakayopokelewa na kufanyiwa kazi ni maombi ya cheti ngazi ya NTA Level 5 tu.

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **18/10/2021** saa **9:30** Mchana

**Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta:-**

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga,  
S.L.P. 22,  
**Mahenge/Ulanga**  
**MOROGORO.**

  
**SAIDA ADAMJEE MAHUGU**  
**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA**  
**H/W-ULANGA**

**MKURUGENZI MTENDAJI <W>**  
**HALMASHAURI YA WILAYA**  
**ULANGA**